# MACHAKOS UNIVERSITY

**University Examinations 2018/2019**

**SCHOOL OF HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES**

**DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES**

**APRIL SESSION EXAMINATION FOR**

**MASTER OF ARTS (KISWAHILI)**

**AKS 503: THEORIES OF LITERARY CRITICISM AND TEXTUAL ANALYSIS**

**TAREHE: 22/8/2019** **MUDA: 2:00 – 5:00 PM**

***MAAGIZO***

***Mtihani huu una maswali matano.***
***Jibu swali la kwanza na yoyote mawili.***

**NB: USITUMIE kitabu/hadithi moja kujibia maswali yote.**

SEHEMU A: (**Lazima**)

1. a) Fafanua uamilifu (functions) wa nadharia ya uandishi? (alama 10)

   b) Kwa kutumia kitabu chochote ulichokisoma katika kozi, hakiki malengo nasibu (unconscious motives) ya mhusika mkuu, yaani ni mambo kiini yapi yanafafanuliwa na ni vipi mambo hayo yanavyojenga muundo au kufafanua kitabu? (alama 20)

**SEHEMU B:**

2. Kwa kutumia msimamo wa Umarx na kitabu KIMOJA chochote kufafanua jibu lako, onyesha njia ambayo(zo) hadithi inadhihirisha na kutuchochea kulaumu nguvu kandamizi. (alama 15)

3. Tathmini mihimili ya kimsingi ya nadharia ya Ufeministi/Unisai, na matumizi yake katika kitabu chochote ulichokisoma katika kozi. (alama 15)

4. "Mtazamo wa Wanaurasimukanuni (Formalists) ni juu ya maana moja ya hadithi na njia moja tu ya kufafanua maana". Jadili ukweli wa dai hili ukiregelea riwaya ya Juma ya *Adhabu ya Mahaba*. (alama 15)

5. "Udenguzi (Deconstruction) zaidi ni njia ya usomaji kuliko kuwa nadharia ya fasihi, na inalenga kuonyesha jinsi hadithi hujidengua au hujikanganya zenyewe". Unakubali? (alama 15)

# MACHAKOS UNIVERSITY

**University Examinations 2018/2019**

**SCHOOL OF HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES**

**DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES**

**APRIL SESSION EXAMINATION FOR**

**MASTER OF ARTS (KISWAHILI)**

**AKS 500: TRENDS IN LINGUISTIC THEORY**

**TAREHE: 23/8/2019** **MUDA: 10:00 – 1:00 PM**

***MAAGIZO***

***Mtihani huu una maswali matano.***
***Jibu swali la kwanza na maswali yoyote mawili.***

1. a) Eleza dhana ya uambishaji katika Kiswahili. (alama 10)

   b) Jadili umuhimu wa uambishaji katika Kiswahili huku ukitoa mifano mwafaka. (alama 20)

2. "Uyeyushaji wa sauti tunapoongea ni lazima kutokea". Jadili hoja hii ukitoa mifano ya Kiswahili. (alama 15)

3. Eleza njia tofauti tofauti za uzalishaji wa maneno katika lugha kuziba upungufu wa msamiati. (alama 15)

4. Jadili urejeshaji wa Kishaji katika Kiswahili na vikwazo vyake. (alama 15)

5. Tathmini ungiosahili (coordination) na ungiotegemezi (subordination) katika Kiswahili. (alama 15)